**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

**Kumb.Na.BA.1/25/01A/7** **21 Oktoba, 2025**

**TANGAZO LA MAREKEBISHO YA NAFASI YA KAZI**

Tume ya Utumishi Serikalini imefanya marekebisho madogo kwa tangazo lake la nafasi za kazi kwa Wizara ya lililotoka tarehe 20 Oktoba, 2025.

Nafasi ya kazi ya Karani Kumbukumbu Daraja la III imeondolewa na badala yake imeingizwa nafasi ya Afisa Takwimu za Afya Msaidizi Daraja la III kama ifuatavyo:

1. **Afisa Takwimu za Afya Msaidizi Daraja la III (ZPSF -10) Nafasi 2 Pemba**

***<u>Sifa za Muombaji:</u>***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 46.
- Awe amehitimu Stashahada ya Takwimu za Kiafya au Taarifa za Kiafya kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

***<u>Jinsi ya Kuomba:</u>***

- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo: **https://portal.zanajira.go.tz** kuanzia tarehe **21 Oktoba, 2025 hadi tarehe 03 Novemba, 2025.**
- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini **www.zanajira.go.tz**.
- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanAjira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-

  **KATIBU,**

  **TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,**

**S.L.P 1587,**

**ZANZIBAR**

- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoiomba.
- Muombaji atakaewasilisha "Progressive Report" au "Statement of Results" pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

**LIMETOLEWA NA:**
**KATIBU,**
**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.**